JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI FURAHIA
S.L.P.1405,

IRINGA
TAREHE, 11/12/2020

KUMB. NA. FSS/2467/FOJI/2020/01

- **Mkuu wa shule : DAVID ELIA KYANDO.**
  Simu no.0717657802 au 0752183065
- **Makamu mkuu wa shule: JUMA LWEHELA.**
  Simu no.0737229282
- **E-mail- furahiasss2467@gmail.com.**

MZAZI/MLEZI WA. .....
ANUANI *(Shule ya msingi atakayo Mwanafunzi)*
.....
S.L.P. .....

YAH: MAAGIZO YA AWALI YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI FURAHIA KIDATO CHA KWANZA MWAKA 2021

Nafurahi kukujulisha kuwa mwanao. **.....** Amechaguliwa kujiunga **KIDATO CHA KWANZA** katika shule ya **SEKONDARI FURAHIA**.

Shule ya sekondari Furahia ipo tarafa ya Isimani, kata ya Malengamakali kijiji cha Usolanga umbali wa kilometa sabini na nane (78km) kutoka Iringa mjini katika halmashauri ya wilaya ya Iringa. Usafiri wa basi kutoka Iringa unapatikana katika kituo cha mabasi cha Iringa mjini (Stendi kuu). Nauli ni shilingi elfu tano (5,000/=) kutoka stendi kuu hadi shuleni.

Muhula wa kwanza wa masomo utaanza tarehe **11/01/2021** ambapo unatakiwa kuripoti shuleni tarehe hiyo kwa mandalizi ya masomo na mwisho wa kuripoti ni tarehe **19/01/2021** (kila mwanafunzi aje na mzazi au mlezi wake anayetambulika (ni muhimu sana) Kutofika shule kwa wakati uliopangwa kunaweza kumpotezea nafasi yake ya masomo.

Mwanao atapokelewa shuleni endapo atasoma vyema maelekezo na kukubaliana nayo na kutimiza mambo yaliyomo kwenye viambata A – F

A. Maelezo Maalumu ya Kujiunga na Shule.
B. Sheria, Kanuni na taratibu za shule.
C. Fomu ya kupimwa kutoka kwa Mganga (Medical examination form).
D. Fomu ya taarifa muhimu ya mwanafunzi.
E. Ahadi/Kiapo cha mwanafunzi.

NB Tunza vizuri na kwa usalama fomu hii ije katika hali ya usafi.

Ni matumaini yangu kwamba mwanao atasoma na kuzingatia maelekezo yote na mzazi/mlezi utamtimizia mahitaji yote kabla ya kuripoti shuleni ili kuepuka usumbufu usio wa lazima. Vile vile mwanao atambue kuwa kama hatojituma katika masomo na kupelekea kupata daraja sifuri kwenye mitihani yake yoyote ile itakayotolewa shuleni, hatua kali zitachukuliwa dhidi yake.

NAKUKARIBISHA SANA

.....
DAVID ELIA KYANDO
MKUU WA SHULE

A: MAELEZO MAALUMU YA KUJIUNGA NA SHULE .

F-01

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI FURAHIA
S.LP.1405
IRINGA

1. SARE ZA SHULE

WAVULANA

i. Mashati mawili (2) meupe yenye mikono mifupi.
ii. Suruali mbili (2) za rangi ya kijani ambazo zinashonwa hapa shuleni. Mwanafunzi asithubutu kushonewa nyumbani hatopokelewa.
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vinavyopigwa brush na vyenye kamba pea mbili.
iv. Soksi nyeupe jozi mbili.
v. Vifaa vya michezo (Raba, T – shirt ya blue, Bukta)
vi. Track suit nyeusi yenye mistari meupe

WASICHANA

i. Mashati (Blauzi) mawili (2) meupe mikono mifupi
ii. Sketi mbili (2) rangi ya kijani yenye marinda box ambazo zinashonwa hapa shuleni. Mwanafunzi asithubutu kushonewa nyumbani hatopokelewa
iii. Viatu vya ngozi vyeusi vinavyopigwa brush na vyenye kamba pea mbili
iv. Soksi nyeupe jozi mbili
v. Vifaa vya michezo (Raba, T – shirt ya blue, Bukta)
vi. Track suit nyeusi yenye mistari meupe

NB

T – shirt zenye nembo ya shule zitapatikana shuleni kama sehemu ya sare ya shule kwa wanafunzi wote

Ikumbukwe kuwa shule ni ya kutwa ila ina nafasi za hosteli kwa wavulana na wasichana, uchangiaji unafanyika kwa makubaliano ya wazazi na kamati ya uendeshaji wa hosteli na kulipwa kwa mwaka. Shule inatoa kipaumbele kwa wasichana kuishi hosteli hivyo mzazi unaombwa kumleta mwanao hosteli kwa ajili ya uangalizi wa karibu na usalama zaidi.

2. MAHITAJI YA DARASANI

i. Madaftari 09 (Counter Book)
ii. Kalamu/Penseli za kutosha
iii. Mkebe wa hisabati (Mathematical Set)
iv. Kamusi ya kiingereza (Dictionary) hii ni **lazima** mwanafunzi awe nayo

3. MAHITAJI MENGINE

i. Kwanja 1 na Mfagio (fagio la chelewa 1)
iii. Jembe na mpini wake.
iv. Ndoo moja ya lita ishirini

ZINGATIO: ***Mahitaji yote yaliyotajwa hapo aje nayo siku ya kuripoti shueni kwa ajili ya usafi wa mazingira***

Tafadhari soma kwa makini maelezo haya na kuyatekeleza kikamilifu

B: FOMU YA SHERIA NA KANUNUNI ZA SHULE.

F-02

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI FURAHIA
S.LP.1405
IRINGA

KANUNI NA TARATIBU ZA SHULE (SHERIA ZA SHULE)

Mwanafunzi anapaswa kufuata na kutekeleza kanuni na taratibu zifuatazo;

MAHUDHURIO.

kuthamini muda wa kuwepo mahali anapotakiwa kwa mujibu wa taratibu za shule au maelekezo kutoka uongozi wa shule.

1. kuwahi kufika shuleni na kuwa mstarini asubuhi
2. kuwepo eneo la shule wakati wote ispokuwa unapopata ruhusa maalumu kutoka kwa mkuu wa shule.
3. kuhudhuria vipindi vyote vya masomo
4. kuhudhuria mikutano halali ya shule kama Baraza la shule, ukaguzi wa uasafi na maandamano.
5. kuitikia miito ya dharura mara moja.
6. kutotoka nje bila ya ruhusa.

HESHIMA.

1. Mwanafunzi anatakiwa kusalimia mwalimu au mtu yeyote anaye mzidi umri anapoingia darasani
2. Mwanafunzi atumie lugha nzuri wakati wote
3. Kushirikiana na kusaidiana na wanafunzi wengine katika kazi
4. Kuthamini na kuheshimu kazi za aina zote
5. Kuitikia mara moja wito wa kengele
6. Kuheshimu bendera ya serikali, picha za viongozi wa vyama na serikali, Nembo ya Taifa wimbo wa Taifa na fedha za Taifa.
7. Kuheshimu taratibu za mkutano, ofisi za shule mali binafsi na mali ya Uma.
8. Kusimama mstari wakati wa kupokea huduma.
9. Kukaa kimya darasani, kutoka inje kwa ruhusa ya mwalimu au kiongozi wa darasa.
10. Kuwa mfano mzuri wa heshima na tabia njema mahali popote ulipo ndani na inje ya shule
11. Kuwaheshimu walimu na wafanyakazi wasio walimu.
12. Baadhi ya tabia ambazo hauruhusiwi mwanafunzi.

A. Kuvuta sigara, kutumia madawa ya kulevya na pombe.
B. Kufuga kucha, ndevu na nywele ndefu.
C. Kuvaa mavazi yasiyo kuwa na heshima.
D. Kugombana, kupigana, kutukanana nk.
E. Uasharati, wizi, utapeli.
F. Imani za kishirikina.
G. Kuwa na tabia ya kiwenda wazimu.

SARE ZA SHULE

Sare ya shule unatakiwa uvae wakati wa;

a) Masomo darasani
b) Unapotoka nje ya shule kwa shughuli za shule
c) Mhadhara wa shule (school baraza)
d) Unapokwenda hospitalini
e) Maandamano.
f) Wanafunzi wanapo safari kuja shule au kwenda kwao wakati wa likizo
g) Kazi za mikono
h) Michezo

Pia;

i) Kofia, viatu vya ghorofa na mapambo haviruhusiwi
j) Nguo ziwe safi wakati wote
k) Lazima kuwa na kitambulisho
l) Kuvaa sare ya kushindia wakati wote
m) Ni marufuku kuhudhuria minadani/gulio ukiwa shule.

MAKOSA YANAYOWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE;

1. Wizi.
2. Uasherati, Ubakaji na Ushoga.
3. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya.
4. Uvutaji wa bangi.
5. Makosa ya jinai.
6. Kupigana au kupiga.
7. Kuharibu kwa makusudi mali ya Umma.
8. Kudharau Bendera.
9. Kuoa au kuolewa.
10. Kupata mimba au kusababisha mimba ndani au nje ya shule.
11. Kutoa mimba.
12. Kugoma, kuchochea na kuongoza au kuvuruga amani na usalama wa watu
13. Kukataa adhabu kwa makusudi.
14. Kutoka nje ya kijiji hiki bila ruhusa ya maandishi toka kwa mkuu wa shule..
15. Kumiliki simu na vifaa vinavyohusiana na simu kinyume na taratibu za shule
16 Kwa mwanafunzi wa hosteli
    a) Kutoroka wakati wa usiku.
    b) Kwenda nje ya mipaka ya shule bila kibali cha matroni au patroni au mkuu wa shule .
    c) Kuvuruga hali ya amani na utulivu .
    d kulala nje ya bweni siku moja au Zaidi bila ruhusa ya mkuu wa shule

17. Wanafunzi wanaotoka nje ;

Nyumba anayokaa ni sehemu ya shule hivyo ni marufuku.

a) Kugeuza kama sehemu ya danguro.
b) Kijiwe cha ulevi uvutaji bangi n.k

.....

DAVID ELIA KYANDO

MKUU WA SHULE

SHULE YA SEKONDARI FURAHIA

C.MEDICAL EXAMINATION FORM

F-03

PRESIDENT'S OFFICE
REAGIONAL ADMINISTRATION AND LOCAL GOVERNMENT AUTHORITY
IRINGA DISTRICT COUNCIL

FURAHIA SECONDARY SCHOOL,
P. O. BOX 1405,
IRINGA – TANZANIA

To be completed by medical officer in respect of all form

FULL NAME.....
AGE.....
BLOOD COUNT (RED AND WHITE) .....
STOOL EXAMINATION.....
URINE MALYSIS.....
SYPHILIS TEST.....
EYE TEST.....
T.B.....
EAR.....
CHEST.....
SPLEEN.....
ABDOMEN.....

ADDITIONAL INFORMATION e.g. Physical or chronicle of family diseases.

.....
.....
.....
.....

I certify that the above named is fit to pursue studies
Signature.....
Designation.....
Section.....
Date.....

N.B

Every student must bring this complete form when coming to school; no student is going to be enrolled without this certificate of physical fitness

D:FOMU YA TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI .

F-04

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA
SHULE YA SEKONDARI FURAHIA
S. L.P 1405,
IRINGA

TAARIFA MUHIMU ZA MWANAFUNZI

1. Jina la mwanafunzi.....Jinsia: ☐ ME ☐ KE
2. Tarehe ya kuzaliwa: | | | | | | | | |
3. Uraia..... Kabila .....
4. Shule ya msingi utokayo ……
5. Kidato alichopokelewa..... Tarehe .....
6. Jina la baba .....
7. Jina la mama .....
8. Anuani ya mzazi au mlezi **S.L.P** ....
9. Namba za simu ya mzazi au mlezi ....., ...
10. Kazi ya mzazi au mlezi .....
11. Wazazi wanaishi pamoja: Ndiyo ☐ Hapana ☐

F:FOMU YA KUKUBALI /KUTAA NAFASI YA SHULE

F-05

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
OFISI YA RAIS- TAMISEMI
HALMASHAURI YA WILAYA YA IRINGA

SHULE YA SEKONDARI FURAHIA
S.LP. 1405
IRINGA

,

A. AHADII KIAPO CHA MWANAFUNZI

Mimi .....
Ambaye nimechaguliwa kujiunga na **SHULE YA SEKONDARI FURAHIA KIDATO CHA KWANZA** Kutoa shule ya msingi ..... mwaka 2021 ninaipokea na **kuikubali/kutoikubali** nafasi niliyo pewa kwamalengo ya kusoma kwa bidii na kufikia malengo yaTaifa kwa Shule ya Sekondari ya Furahia
.

Ninatambua kuwa nafasi hii ni adimu, nyeti na ya upendeleo kwangu ili niweze kusoma na kufanya vizuri katika masomo nikiwa na tabia na mwenendo mwema kwa ajili ya Taifa langu la Tanzania, familia yangu na kwa ajili yangu pia.
Nina amini kuwa vitendo vyovyote vinavyopelekea uzembe katika kufanikisha makusudio haya ni hujuma kwa Taifa langu, familia yangu na kwangu pia. Hivyo ninaahidi kuwa, nikiwa hapa shuleni:

i. Nitasoma kwa bidii kwa malengo ya kufanya vizuri katika masomo yote.
ii. Nitashika na kufuata sheria na taratibu zote za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa na zingine zitakazokuwa zikitolewa mara kwa mara.
iii. Sitajihusisha na vitendo vyovyote vya utovu wa nidhamu nikiwa hapo shuleni. Ikiwemo utoro wa vipindi darasani.
iv. lkiwa nitakiuka sheria kanuni na taratibu za shule kama nilivyo zisoma na kuzielewa, nitakubali kurudishwa nyumbani kumwita mzazi/ mlezi wangu. au kufukuzwa shule pale inapobidi.

Saini ya mwanafunzi ..... Tarehe.....

B:SEHEMU YA MZAZI/ MLEZI

Mimi ..... ninakubal/sikubali mtoto wangu ..... Kupata na kupokea nafasi katika shule ya sekondari Furahia mwaka 2021.Ninaahidi kumpatia mahitaji yote ya shule kama ilivyo katika maagizo ya kujiunga na shule. Ninakuhakikishia kuwa nitashirikiana na shule wakati wote kuona kuwa mwanangu anatekeleza wajibu wake kwa shule na kwa Taifa.
Anuani yangu ya kudumu ni **S.L. P .....**, **.....**.
Simu …… …….....
lwapo nitapata uhamisho wa kubadili makazi au anuani nilazima nitaijulisha shule kwa maandishi.

Saini ya Mzazi/Mlezi ..... Tarehe .....

AHSANTE